**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATOMBO 2024

**APRILI, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS–TAMISEMI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 0714 907 572**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0716 600 067**

**Mwandamizi Taaluma:0655 182 992**

**Matron: 0714806267/0762 412 377**

**ShuleyaSekondariMatombo**

**S.L.P 749**

**MorogoroTarehe**

**26/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi........................................... .....**
**S.L.P............**
**..................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATOMBO HALMASHAURI YA WILAYA MOROGORO MKOA WA MOROGORO MWAKA2024/25**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya HGL/HKL/HKfa/HGli (Kata isiyohusika)

Shule ya Sekondari Matombo ipo umbali wa Kilometa 64 Kusini mwa Mji wa Morogoro Usafiri wa basi kutoka mjini Morogoro unapatikana katika kituo chamabasi Msavu au Karoleni Nauli ni Shilingi 8,000/= kwa gari.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 29 au 30/06/2023 Mwisho wakuripoti ni tarehe 13/07/2023.

## 2. Mambomuhimuyakuzingatia:-

### 2.1 Sareza Shule

Sare ya shule hii ni:

1. Aje na sketi ya dark bluu mbili (02) za rinda box yenye urefu kufikia usawa wa kifundo Cha mguu. Au anaweza kuzipata kwenye duka la karibu na shule kwa Tsh 25,000/= kwa pea moja.
2. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yakiwa na nembo ya shule ya sekondari Matombo. Au anaweza kuzipata kwenye duka lililopo karibu na shule kwa gharama ya Tsh 12,000 (kwa shatimoja).
3. Aje na hijab (kijuba) ya shule ya rangi nyeupe na ya Kushindia ya rangi ya bluu zote zifunike kifua cha mwanafunzi pia ziwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. Au anaweza kuzipata kwenye duka lililopo karibu na shule kwa gharama ya Tsh 15,000/- kwa pea moja.
4. Aje na Sare ya michezo ya track suit ya dark blue pea moja iliyochapwa Au anaweza kuzipata kwenye duka la karibu na shule kwa gharama ya Tsh 30,000/= **ZIKIWA NA NEMBO YA SHULE NA NAMBA YA UTAMBULISHO KILA MWANAFUNZI.**
5. Aje na Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
6. Aje na Soksi jozi mbili nyeupe;
7. Aje na Sweta la dark bluu la uzi wa kufumwa.
8. Aje na nguo ya kushindia sketi mbili za visanduku vya blue na nyeupe ya rinda box. AU anaweza kuzipata kwenye duka la karibu na shule kwa gharama ya TSH 20,000/=
9. Aje na Tisheti moja au mbili za form six za rangi ya bluu yenye nembo ya shule ya sekondari Matombo. Au anaweza kuzipata kwenye duka la karibu na shule kwa gharama ya Tsh 12,000/ kwa kila moja.

**Muhimu: Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa Sare iliyo tofauti katika rangi, mshono, nembo na kipimo kinyume na maelekezo yaliyopo kwenye fomu hii.**

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo**

**shuleni:-**

Madaftari ya kaunta book tisa au zaidi

1. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka na rulled paper (karatasi za mistari mbili (02) kwa mwaka; Au Karatasi zote zinaweza kupatikana kwenye duka karibu na shule kwa bei nafuu.
2. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa/au wasiliana na ofisi ya taaluma ikiwa utahitaji msaada zaidi.*);
3. Scientific Calculator 1(wanafunzi wa Geography)
4. Godoro lenye vipimo vya 2.5x6
5. Shuka za rangi ya pinki Jozi2, blanket1, mto na foronya ya mto1, chandarua1 cheupe; Nguo za ndani za kutosha;
6. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijikonakikombe);
7. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi)zenye mifuniko za kuogea.
8. Aje na Kwanja 1, jembe1, reki1, sabuni ya maji lita 2, fagio la ndani (soft broom) 1, Fagio la chooni (Hard brooom) 1, Toilet brush 1, ufagio wa Chelewa 1, ndoo kubwa Moja (01) lt 2 na squeezer 1.

## Michango mbalimbali

Shule ya Sekondari Matombo ni ya Bweni, hivyo mwanafunzi unatakiwa kuweka michango ifuatavyo kwenye akaunti ya shule kabla ya kuripoti shuleni na ufike na risiti ya benki au risisti ya kielekriniki kuthibitisha malipo yako.

| Na | Aina yaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | KitambulishochaShule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Malipo yafanyike kupitia akaunti namba 22101100129 jina Matombo Secondary School Benki ya NMB**

## Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### Sheria na Kanuni za Shule

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana naratiba yashule;
3. Kushirikikwakikamilifumasomoyausiku(Preparation);
4. Kuwahikatika kilashughulizashuleutakazopewa;
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
9. Kutunza mali za shule;
10. Ni marufuku mwanafunzi kumilikivifaavyenyenchakalinadawabilaidhini yadaktari; na
11. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

1. **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyoteile,nahakunamtumishianayeruhusiwakutunzasimuyamwanafunzi;**
    1. **MwanafunziawaposhuleniatatakiwakulalakwenyeBwenialilopangiwanakitandaalichopangiwa.Nimarufukumwanafunzi kulalakitandakimojanamwenzakeaukuishikwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumikanamwanafunzimmojatu;**
    2. **MwanafunziataruhusiwakurudinyumbanikwaruhusanakibalimaalumtokakwaMkuuwaShule.(MsibaauUgonjwa**).

b. **Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi yasiku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwaujumla;
v. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa msuko wowote. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya; kama Uvutaji wasigara, bangi na kadhalika.

viii. Uasherati,mahusiano ya jinsia moja,kuoa au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule bila kufuata utaratibu uliwekwa na shule;
xiii. Kudharau Bendera yaTaifa;
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

- Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
- Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
- Picha nne za wazazi au ndugu wa karibu wa mwanafunzi wasiozidi 04 (picha moja kwa kila mzazi/ndugu wa karibu iwe ya size ya Passport) wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za Simu.

- Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

THE HEADMISTRESS
MATOMBO SEC. SCHOOL
P. O. B0x 749
MOROGORO

**Jina la Mkuu wa Shule MARIAM R MADAMBA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**ZINGATIA:**

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

**Mkuu wa shule 0714 907 572**
**Makamu Mkuu wa Shule 0716 600 067**
**Mwandamizi Taaluma 0655 182 992**
**Mwandamizi Malezi 0762 412 377**

**Kiambatanisho cha mshono wa sketi**








MATOMBOSECONDARYSCHOOL,P
.O.Box749,
**MOROGORO.**
DATE ...........................

Ref.No.............................................

**PART A:-**
TotheMedicalOfficer,
.........................................................
.........................................................
.........................................................

**REF:**
**...........................................................................................................................................................**
Please examine the above named student as to her physicaland mental fitness for being student.
Eachdefectwillhinderagirlfor SecondarySchools'education.

1. a). Eyesight
   b). Hearing
   c). Limbs
   d). Speech
   e). Venereal disease
   f). Leprosy
   g). Epilepsy

Neurosis
Other serious diseases
Pregnancy

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**)

I have examinedthe abovenamed student and confirmthat she is physically fit/notfit for a full time Secondary School Education.

a). Eyesight.......................................
b). Hearing..........................................
c). Limbs ............................................
d). Speech............................................
e). Venereal diseases
f). Leprosy............................................
g). Epilepsy............................................
h). Neurosis............................................
i). Other serious diseases........................
j). Pregnancy…………………………..

Name........................................................... Signature........................... Date...........................

**STATION**............................................................ **DESINATION**.................................................
**N.B.**I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.

**FOMUYAHISTORIAYAMWANAFUNZI**

1.JINA LA MWANAFUNZI.........................................................................................................

2.JINA LA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI....................................................................

3.JINA LA SHULE ANAKOTOKA..............................................................................................

4.TAREHE YA KUZALIWA.........................................................................................................

5.KATA ANAYOTOKA MWANAFUNZI.......................................................................................

6.WILAYA ANAYOTOKA MWANAFUNZI...................................................................................

7.MKOA ANAOTOKA MWANAFUNZI........................................................................................

8.KABILA...........................................................................................................................

9.URAIA.............................................................................................................................

10.DINI/DHEHEBU...............................................................................................................

11.ANUANI YA MZAZI/MLEZI.................................................................................................

NAMBA YA SIMUYA MZAZI/MLEZI. -NYUMBANI.......................................................
-OFISINI.............................................................

e-mailadress......................................................................................................................

NAMBA YA WHATSAPP KWA AJILI KUTUMA MATOKEO: (Inaweza kuwa ya ndugu wa karibu)

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

MAJINA MANNE YA NDUGU WAKARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARURA ITATOKEA:-

| Na | JINA | UHUSIANO | ANAKOISHI | NAMBAYA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 01. | | | | |
| 02. | | | | |
| 03. | | | | |
| 04. | | | | |

**MATOMBO SECONDARY SCHOOL-ORODHA YA VITABU VINAVYOHITAJIKA)**

**(Baadhi ya vitabu vinaweza kupatikana Katika duka lililopo jirani na shule)**

**GEOGRAPHY PAPER1**

Principles of Physical Geography-by F.JMonkhouse

Acomprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School-by D.T Msabila

Practical Geography for Africa by John M.Prichard

Landforms in Africa–An introduction to Geomorphology–by Colin Buckle

Africa–byJ.M.Prichard

Practical Geography for Alevel–by Francis Mnyawi

Physical Geography By Haruna Masenza - vinapatikana shuleni
Practical Geography by Haruna Masenza -vinapatikana shuleni

Human and Economic Geography By Haruna Masenza - vinapatikana shuleni
Human and Economic Geography–by Gohcheng&Morgan

Advanced Level geography Course book–byTanzania Institute of Education (TIE)

An Integrated Focal regional study on Human and Economic Geography

Advanced level paper 2-by D.T Msabila

**ENGLISH LANGUAGE**

English language form 5&6 By Mgonja - vinapatikana shuleni
Literature in English form 5&6 By Mgonja - vinapatikana shuleni

**NOVELSANDSHORTSTORIES**

Chinua Achebe–Aman of the people

Ayi Ewei Armah–The Beautiful ones are not yet born

Soga–His Excellence the head of state.

**PLAYS**

I will marry when I want by Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Miri

An Enemy of the people by H.Ibsen

The Caucasian Chalk Circle by B. Bretch

iv.Betrayal in the city by F.Imbuga

**POETRY**

Tanzania Institute of Education– Selected poems

David Cook etal–Poems from East Africa

**Orodha hii ya vitabu vya KIINGEREZA ni kwa wanafunzi wanaosoma HGL na HKL tu. Kwa wanasoma mchepuo mpya wa HGLi na HGfa wasiliana na Idara ya taaluma kwa ajili maelekezo zaidi baada ya kupokea mwongozo.**

**HISTORY**

History paper Two by Leonard Revelian -vinapatikana shuleni
Advanced Biology by Abubakar said -vinapatikana shuleni

Rodney,W–How European Underdeveloped Africa

Nyirenda,H.D–Africain World History–Alevel Notes

Nabudere,D.W–Essay on theTheoryandPracticesofImperialism

LeninV.I.Imperialism the highest stage of capitalism

Nyangwine,N.advancedLevel–History Notes, Selected topics for paper 1&2

World Map, Africa Map, East Africa Mapand Tanzania Map.

**KISWAHILI: I**

Historia ya matumizi ya Kiswahili, Mbunda
Msokile (1992), Education Publishers and Distributors Ltd
Kiswahili sekondari.Taasisi ya Ukaguzi Mitaala (1958)
Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo James S.Mdee(1988),DUP
Kiswahili kidato cha Tano.TIE

**KISWAHILI:II**

Fasihi. SenkoroF.E.M.K.(2011)KauttuLimefedDSM)(2011)
Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI –DSM) Toleo lapili

**RIWAYA**

Kufikirika Shaaban Robert T. Mkuki na Nyota
Publishers Dares Salaam,(2003)
Mfadhili, Hussen Tuwa Macmillan AIDAN (2007)
Usiku Utakapokwisha– Mbunda Msokile, Macmillan.

**USHAIRI**

Mapenzi bora Shaaban Robert, Mkuki na Nyota Publishers(2007).
Chungu Tamu T.A. Mvungi,TPH Dares salaam(2004).
Fungate ya Uhuru, Mohamed S Khatib
Kimbunga, Haji GORA HAJI TUKI Daressalaam,(2003).

Kumbuka:

Vitabu ni muhimu kwa mafanikio ya kitaaluma ya mtoto. Mzazi hakikisha mwanao ananunua angalau vitabu viwili katika orodha kwa kila kundi kulingana na mchepuo wake. Ikiwa utapata changamoto katika majina na waandishi wa vitabu wasiliana na mwalimu wa taaluma kupitia namba zilizopo katika fomu hii.

11

**KIAMBATISHO: SARE ZASHULENAGHARAMA ZAKE**

Uniform zinazopatikana shuleni na beizifuatazo:

Skirtblue (moja)-25000/=Shatijeupe(moja)12000/=T-

shirtbluebahari (moja)-12000/=

Track suit ya michezo  Tsh 30000

Hijabu white & blue (moja) 15000/=

skirt shamba (moja) 20000/=

Nembo 2 Tsh 10000/=

(Mwanafunzi anashauriwa kuwa na pea mbili kwa uniform zote zilizoorodheshwa hapo juu)

Mwanafunzi atakayetaka kununua sare zinazopatikana kwenye duka lililo karibu na shule aje na pesa mkononi, zisiwekwe kwenye akaunti.